

Taasisi ya Thirldmill

Beji ya Uinjilishaji

Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa wote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Mathayo 28:18-20

Katika Injili ya Mathayo, haya ni maneno ya mwisho ya Yesu kabla ya kupaa kwenda Mbinguni. Katika maisha yako, fikiria ni nini ambacho ungeweza kusema kwa wale waliokaribu na wewe kama ungekuwa na nafasi ya kusema maneno ya mwisho. Maneno hayo yangekuwaje? yasingehusu hali ya hewa, kazi yako, au matokeo mazuri ya timu unayoipenda. Yatakuwa mambo ambayo yako ndani kabisa ya moyo wako. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa Yesu. Alisema maneno ambayo yalikuwa muhimu kwao kuyasikia. Kuwanya watu kuwa wanafunzi ndilo lilikuwa jambo muhimu zaidi kwake. Utume wa Yesu ulikuwa kueneza Injili ya Ufalme and kufanya watu kuwa wanafunzi, yaani wafuasi wake, na hiyo ndiyo ilikuwa hamu yake kubwa. Hatua ya kwanza katika kuwafanya watu kuwa wanafunzi ni kupitia uinjilishaji.

Katika beji hii, mtajadili kuhusu maana ya kuhubiri Injili kulingana na mazingira yako na jinsi ya kufanya hivyo. Aidha, utakuwa na fursa ya kushuhudia ushuhuda wako kwa mtu ambaye hamjui Yesu.

Vipengele vya Beji:

Uwasilishaji wa Injili – Utachagua mambo ambayo unaweza kuyajumuisha wakati wa kuhubiri Injili.

Ushuhuda Binafsi – utajadili namna ya kutumia ushuhuda wako katika kuhubiri Injili

Uzoefu wa Kuinjilisha – utatumia uzoefu wako kuwahubiria Injili watu mwingine.

Mada za Kujadili:

1. Jibu swali hili kwa kutumia maneno yako mwenyewe: Injili ni nini? Jadili jibu lako katika kikundi chako.
2. Uinjilishaji unaonekanaje katika nchi yako? Watu wanaelewa vipi? Ni mfumo gani wa kawaida wa uinjilishaje uliozoeleka katika nchi yako?
3. Mambo gani ya muhimu yanapaswa kujumuishwa katika uwasilishaji wa Injili? Orodhesha mambo hayo, kisha chagua mambo 6 ambayo ni ya muhimu zaidi.

4. Ni njia gani ya kuhubiri Injili yenye ufanisi zaidi katika nchi yako? Je, ni ile ya kuwahubiria watu usiowafahamu, au watu ambao tayari una mahusiano nao?
5. Unahubiri vipi Injili kwa mtu unayemfahamu dhidi ya mtu usiyemfahamu?
6. Je, kuhubiri Injili ni hatari katika nchi yako? Na je, hali hiyo ina athari gani katika kuhubiri kwako Injili kwa watu wengine?

Ushuhuda Binafsi:

Kila mtu ana ushuhuda binafsi wa namna ambavyo alikata shauri na kumwamini Yesu Kristo kuwa mwokozi wao. Ushuhuda wako ni dhana yenye nguvu sana ambayo unaweza kuitumia muda wowote kuleta mabadiliko katika maisha ya mtu. Firiki jinsi ambavyo ulimjua Yesu kama mwokozi wako. Andaa ushuhuda mfupi, kama dakika 3 tu ambao unaweza kuwashuhudia watu wengine.

Hatua tatu za kukusaidia unapotaka kuandaa ushuhuda wako.

Hatua ya 1: Maisha yako kabla ya kumjua Yesu yalikuwaje, na je, maisha yako ya awali yanaweza kuwa na uhusiano gani na mtu unayeongea naye?

Hatua ya 2: Mazingira yaliyokuzunguka yalichangia vipi kwako wewe kumjua Yesu na hata kumwamini? Ni kitu gani kilikufanya uone kwamba Injili ni kweli?

Hatua ya 3: Ni kitu gani kilichobadilika katika maisha yako baada ya kumwana Kristo ambacho kinaweza kuwa na manufaa kwa mtu mwingine?

Mambo ya Kufanya:

1. Andika ushuhuda wako, kariri na kisha umshirikishe mkufunzi wako na wengine katika kikundi chako.
2. Shuduia ushuhuda wako kwa mtu ambaye siyo Mkristo.
3. Jadiliana na mkufunzi wako pamoja na wanakikundi wenzako jinsi ilivyokuwa. Kitu gani kilienda vizuri? Na ni kitu gani unaweza kuboresha?

Vigezo vya Beji:

Utatunukiwa Beji hii na tasisi ya Thirdmill kama sehemu ya Cheti cha Misingi baada ya kufuzu vigezo vyote vya Beji vilivyoko kwenye **mambo ya kufanya** kwa uaminifu, na **uthabiti**, kwa kufuata **vipengele vya Beji**, na muktadha wa **mada zilizozungumziwa** katika kipindi chote cha kozi.